

Maswali

1. Baba alikuwa na wana wangapi?
2. Mwana mdogo alimuuliza nini?
3. Mwana mdogo alienda wapi?
4. Alifanyia nini hizo pesa za babake?
5. Alifanya nini alipomaliza kutumia pesa zake zote?
6. Mwana mdogo alikumbuka nini juu ya watumishi wa babake?
7. Aliamua kufanya nini?
8. Nani alikuwa akimngojea mwana mdogo?
9. Babake alifanya nini alipomwona mwanae mdogo?
10. Nani alikasirikia mwana mdogo alipokuja nyumbani?

Majibu

1. Baba alikuwa na wana wawili.
2. Mwana mdogo alitaka babake ampe pesa
3. Mwana mdogo alienda kwa nchi geni
4. Alitumia pesa za babake zote.
5. Alipomaliza kutumia pesa zote, alienda kulisha nguruwe.
6. Mwana mdogo alikumbuka watumishi wa babake waliokuwa na chakula kingi cha kula.
7. Aliamua kwenda nyumbani.
8. Baba alikuwa akimngojea mwanawe mdogo.
9. Alipomwona mwanawe mdogo, alimkimbilia kukutana naye.
10. Mwana mkubwa alikasirika wakati nduguye alikuja nyumbani.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

39 Mwana aliyerudi

Marejeo

Luka 15:11—32

Kiini cha somo

Kuonyesha huruma ya Mungu kwa watoto wake. Mungu hutusamehe wakati wowote tukitubu

Maneno maalum

1. Wana wawili + mbali + nchi
2. Tumia + njaa + nguruwe + watumwa
3. Baba + angalia + kimbilia + kutana
4. Ndama mnono + potea + patikana
5. Muziki + cheza + mwana mkubwa + kasirika + kufa + hai

39.1 Mara nyingi Yesu alifundisha watu akitumia hadithi. Mara hii kwa hizo hadithi zake anataelezea akitumia mtu aliyekuwana wana wawili.


Siku moja mwana mdogo alienda kwa babaye akasema, “Baba, nipe pesa zangu nitakazopata ukifa.” Baba alimpa hizo pesa. Baada ya muda mfupi yule kijana mdogo alichukuwa pesa zote alizopewa na babaye na kusafiri nchi ya mbali. Kwa hiyo nchi geni, alikaa raha mstarehe, akila, akinywa na kutumia pesa zake zote kwa chochote alichotaka.

39.2 Baada ya kutumia hizo pesa zote, kulikuwa na njaa kwa hiyo nchi geni. Alikuwa na njaa kwa hiyo nchi geni. Alikuwa na njaa kwa sababu hakubaki na pesa zozote. Alienda kumfanyia mkulima fulani kazi ya kumlishia nguruwe.

Huyu kijana alikuwa na njaa sana akataka kula chakula cha nguruwe. Alianza kufikiria juu ya babake na chakula kilicholiwa na wafanya kazi.

Akajizungumzia, “Watumwa wa babaangu wako na chakula cha kutosha wanakula mpaka kinabaki. Na hapa mimi ninakufa kwa njaa.”

Akaamua, “Nitarudi kwa babaangu. Nimwambie vile nimekuwa muovu. Nitamuuliza anifanye kama mmoja wa watumwa wake.”



39.3 Kwa hivyo huyo mwana mdogo alirudi nyumbani kwao na kuenda kwa babake. Ingawaje tangu huyo mwanawe mdogo aondoke, babake alitamani amurudie. Kabla afike nyumbani babake alipomwona kwa umbali akamkimbilia na kumlaki.

Mwanawe alisema, “Baba nimekuwa muovu na sistahili kuwa mwanao.” Lakini babake alimkumbatia na kumbusu. Alipaza sauti akiita watumwa, “Mletee nguo nzuri na mumvalishe mwanangu. Tena mumvalishe pete na viatu miguuni.”

39.4 Kwa hivyo watumishi walifanya walivyoambiwa. Babake aliendelea kusema huku akimpeleka kwa nyumba, “Leta ndama mnono hapa. Muue, tukule, tufurahie. Kwa sababu mwanangu alikuwa amekufa lakini ako hai tena. Alikuwa amepotea lakini amepatikana.” Kwa hivyo wakawa na karamu.

39.5 Kijana mkubwa alikuwa shambani. Alipokuwa akikaribia nyumbani, alisikia muziki na michezo. Baba yao alitoka na kumtaka aje ndani amwone kakake. Kijana mkubwa aliambia babake, “Nimekufanyia kazi kwa miaka mingi. Nimekueshima mda huu wote. Haujawahi kunipa ndama ili nifanye karamu na marafiki wangu. Lakini huyu mwanao aliyetumia pesa zako kwa nchi ya mbali, alipokuja tu umemuia ndama mnono.”

Babake alimjibu, “Mwanangu, umekuwa na mimi kila siku, na kila kitu nilichonacho ni chako. Ilikuwa vyema tusherehekee na tufurahi kwa sababu nduguyo alikuwa amekufa na amefufuka, tena alikuwa amepotea na sasa amepatikana.”

Mungu, Baba aishiye mbiguni yutayari wakati wote kuwasamehe watoto wake wakimrudia na wasema tusamehe.